**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# HALMASHAURI YA JIJI MBEYA

---


*Baruazoteziandikwekwa*:

**Simu; Mkuu wa shule:** +255 768 858 548

Mkam mkuu shule +255 755 105 938

Mwandamizi Taaluma +255 754 308 684

Matroni + 255 754 072 351

Shule ya Sekondari Mbeya,

S. L. P. 372,

**MBEYA.**


Tarehe ……………….

**YAH: MAELEKEZO KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MBEYA KIDATO CHA TANO HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA MKOA WA MBEYA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya …….……

Shule ya Sekondari Mbeya ipo umbali wa Kilometa **1.5** kutoka stendi kuu ya mabasi jijini Mbeya. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Nauli ni Shilingi **2,000** /= kwa pikipiki na Shilingi **2,000=** kwa bajaji.

**2.** Yafuatayo ni maagizo ya kutimiza kabla ya kujiunga na shule hii;

a. Jaza fomu ya kukubali kujiunga na shule hii iliyoambatanishwa (tazama KIAMBATANISHO E). Ijaze kikamilifu iwapo umekubali nafasi hii na iwapo utakubali kufuata masharti/kanuni/taratibu/ na sheria za shule hii kama KIAMBATANISHO A kinavyoonyesha.

b. Nenda kwa Daktari wa Hospitali ya serikali akupime na ajaze fomu ya “medical examination” iliyoambatanishwa (tazama KIAMBATANISHO H)

c. Jaza fomu ya **“KUANDIKISHWA SHULENI NA HABARI ZA MWANAFUNZI/MZAZI/MLEZI”** (tazama KIAMBATANISHO G).

d. Kamilisha fomu ya uthibitisho wa uraia kwa Mkuu wa Wilaya unakotoka (tazama **KIAMBATANISHO F**) au leta kivuli cha cheti cha kuzaliwa kuthibitisha kwamba wewe ni raia wa Tanzania.

e. Fomu zote zilizotajwa hapo juu ufikenazo shuleni na kumkabidhi Makamu Mkuu wa Shule.

**3.** Pamoja na barua hii naambatanisha sheria, kanuni na taratibu za shule. Wewe pamoja na mzazi/mlezi wako mnatakiwa kusoma kwa makini sheria, kanuni na taratibu zote zilizoainishwa na ikizingatiwa kuwa kigezo cha maendeleo ya kila mwanafunzi Atakayejiunga na shule hii kitalenga katika maendeleo ya **TAALUMA** na **NIDHAMU BORA** pamoja na kazi za elimu ya kujitegemea.

**4.** HONGERA **KARIBU SANA** Mbeya Sekondari




NAKALA;

Afisa Elimu wa Mkoa
S. L. P 754,
**MBEYA**

Afisa Elimu Jiji,
S. L. P 149,
**MBEYA.**

## KIAMBATANISHO A.
## SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:** i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro; iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**MAHITAJI YA LAZIMA SHULENI**

**SARE YA SHULE A. WAVULANA**

i. Suruali mbili ya rangi nyeusi moja na rangi nyingine mpja (**angalia kiambatanisho/atashonewa shuleni**) na yenye turn up isiyobana

ii. Mashati mawili yenye mikono mirefu yasiyobana aina ya tetroni. Mashati yote lazima yawe marefu yanayoweza kuchomekewa ndani ya suruali. Pia Suruali iwe na mfuko mmoja wa nyuma ya suruali usio na mfuniko.

iii. Jozi (pair) mbili za viatu vyeusi vya kamba. Visiwe na visigino virefu "ghorofa" au soli nene kupita kiasi. Viwe viatu vya kawaida vya heshima visiwe vya "ajabu". Aidha, huruhusiwi kuvaa raba au buti.

iv. Soksi ndefu rangi nyeusi

v. Sweta rangi ya kijani kibichi iliyoshonwa vizuri isiwe ya wazi (not open) iwe na "V – Shape", sehemu ya shingo. Uje nalo.

vi. Tai rangi ya suruali.

ix. T-shirt utanunua ukifika shuleni

**b. WASICHANA**

i. Mashati mawili meupe yasiyobana aina ya tetroni mikono mirefu, yawe marefu kuweza kuchomekea

ii. Tai rangi ya sketi

iii. Jozi mbili za viatu vyeusi vya kamba na visivyo na visigino virefu au (ghorofa) au soli nene kupita kiasi pia zisiwe raba

iv. Soksi ndefu (stockings) nyeupe jozi mbili au zaidi

v. Sweta rangi ya kijani kibichi iliyoiva na kushonwa vizuri isiwe ya wazi iwe na "V – Shape" sehemu ya shingo (angalia kiambatanisho)

vii. Sketi ya rangi nyeusi moja na rangi nyingine nyingine moja. (**angalia kiambatanisho/atashonewa shuleni**) ziwe ndefu mpaka kwenye kisigino na ziwe za rinda boksi

viii. Shamba dress ni gauni rangi ya ugoro vipimo kama sketi ya shule.

ix. Blanketi moja zito

x. Hijaabu nyeupe kwa Waislam isiyo na urembo kwa ajili ya darasani na ya ugoro kwa ajili ya kushindia

xi. T-shirt utanunua ukifika shuleni

xii. Tochi ya kawaida au ya solar

xiii. Taulo au kanga kwa ajili ya kuogea

- Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sare kinyume na vipimo rangi na aina ya kitambaa tulichokielekeza hatapokelewa.

KIAMBATANISHO B

## MICHANGO MBALIMBALI

### a) Wasichana (Bweni)

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

### b) Wavulana (kutwa)

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 35,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **50,000/=** |

**N.B Malipo** yote ya michango yafanyike Benki ya **NMB A/C No. 61006600286** MBEYA **SEKONDARI** kisha uje na bank pay in slip.

**MAHITAJI MENGINE**

**A. VIFAA VYA TAALUMA**

i. Counter books quire 4. Zisizopungua nane kwa ajili ya notisi za masomo darasani
ii. File moja (spring file) rangi ya NJANO kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi
iii. Picha ndogo 3 za passport size
iv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
v. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne ( Result Slip)
vi. Rimu mbili ya karatasi za "photo copy" A-4 size
vii. Scientific calculator kwa wanafunzi wa Tahasusi ya EGM, PCM na HGE, PMCs
viii. Mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set), "pen" na "pencil" n.k
ix. Vitabu vya ziada kwa ajili ya kujisomea binafsi
x. Graph pad moja.

B. VIFAA VYA MICHEZO

i. Truck suit isiyobana fully rangi NYEUSI yenye mistari mieupe (Adidas)
ii. Raba rangi nyeupe
iii. T-shirt ya blue
iv. Bukta rangi ya blue

**N.B**
Weka alama yako kwenye vifaa vyako vyote

C. VIFAA VYA USAFI

i. Fagio moja ya nje aina ya chelewa kwa ajili ya usafi na
ii. Mopa moja
iii. Soft broom moja
iv. Jembe lenye mpini
v. Brash ngumu yenye mpini mfupi kwa ajili ya kusafishia sinki la chooni.
vi. Ndoo moja kubwa lita 20
vii. Ndoo moja ndogo lita 10 kwa wasichana kwa ajili ya matumizi binafsi bwenini.

**KIAMBATANISHO C**

Tarehe……………

e-mail:*jijimbeya2010@yahoo.com*

KUMB Na…………………..……… Ndugu……………………………..….

**YAH: KUJIUNGA NA HOSTEL**

Nafurahi kukujulisha kuwa mtoto wako

….……………………………………………………….. Amechaguliwa kuingia kidato cha tano (5) na atakaa katika HOSTEL ya shule na kufuata sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa.

Aidha uongozi wa shule utajitahidi kuhakikisha kuwa mwanao anafundishwa vizuri na kumlea ipasavyo, hata hivyo mafanikio katika taaluma na nidhamu yatategemea jinsi wewe mzazi/mlezi utakavyojenga utamaduni wa ushirikiano na uongozi wa shule katika kufuatilia mwenendo, tabia na maendeleo ya taaluma ya mwanao. Tafadhari mwanao aje na barua hii pamoja na viambatanisho A, B na C siku itakapofungua shule rasmi tarehe _____________. Aidha tafadhari zingatia tarehe rasmi ya kufungua shule ambayo mwanao hana budi kuripoti. Tarehe ya mwisho yakupokelewa hostelini Tarehe ___________ Mazingira ya hosteli ni mazuri na shule imezungushiwa uzio kwa usalama wa wanafunzi na mali za Shule.

Pamoja na barua hii tuna ambatanisha:

a. Sheria / kanuni za hosteli (bweni) (appendix A) pamoja na sheria za shule
b. Mahitaji muhimu ya mwanafunzi wa hosteli (bweni) ( appendix B)
c. Fomu ya utii wa sheria na kanuni za hosteli (Appendix C)



## KIAMBATANISHO D

**MAHITAJI YA LAZIMA YA SHULE**
**MALAZI NA CHAKULA KWA WASICHANA**

- Shule itatoa huduma ya chakula malazi, kwa kuzingatia hali halisi ya Mtanzania wa kawaida. Hivyo, kila mwanafunzi atapaswa kuishi kwa amani wakati wote wa masomo.

  **N.B** Shule haitoi chakula maalumu (special diet) kwa wanafunzi wenye matatizo ya afya ya kudumu

- Sanduku liwe la chuma (tranka). Ni lazima lifungwe kwa usalama
- Bed covers (shuka) jozi (pair) Meta mbili na nusu aina ya rangi ya pinki. Kipimo kiwe kamili ili kufunika kitanda chote
- Pluneck nyeupe kwa ajili ya wagonjwa wa kifua/pumu
- Blanketi zito (kwa sababu ya baridi ya Mbeya), mto wenye foronya ya rangi ya pinki, taulo, n.k
- Godoro futi 3x6 au uje na Tshs 10,000/= kukodi godoro kwa muhula
- Vifaa vya chakula; sahani, kikombe, kijiko, bakuli, n.k
- Ndala za kuogea ziwe za rangi ya blue

**ZINGATIA** Vifaa *vyote vitakaguliwa siku unayoripoti shuleni*

**KIAMBATANISHO E**

**SHULE YA SEKONDARI MBEYA** FOMU
**YA KUKUBALI**

1. Mimi ……………………………………………………………. msichana/ mvulana, ninakubali kuingia kidato cha …………… Shule ya Sekondari Mbeya kama mwanafunzi wa kutwa/ hosteli tarehe ……………………… nitafika shuleni bila kuchelewa.
2. Nitatii sheria za shule na nitaishi kwa amani. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea.
3. Sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
4. Saini ya mwanafunzi …………………… Tarehe ……………………………………

Sehemu ya mzazi/ mlezi:

1. Mimi ………………………. ninakubali mtoto wangu……………………. asome katika Shule ya Sekondari Mbeya kuanzia tarehe………….
2. Ninaahidi kulipa ada na michango na pia kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kuwa navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya kujiunga na shule.
3. Ninakuhakikishia kwamba nitamuonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi za kujitegemea.
4. Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubaliwa kuingia katika shule ya Sekondari Mbeya kama mwanafunzi wa kutwa/ hosteli na ataendelea hivyo hadi kumaliza kidato cha sita.
5. Anuani yangu ya kudumu ni:

   ………………………………………………

   ………………………………………………

   Simu No: ………………………..………. (Ofisini)

   Simu No: …………………………..……… (Nyumbani)

   Mobile……………………

6. Sahihi……………… Tarehe ………………….

**KIAMBATANISHO F.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI JIJI MBEYA**

Mkoa wa:………………………………… OFISI YA MKUU WA WILAYA,

WILAYA YA………………

S. L. P. ………………….

TAREHE …………

Mkuu wa shule,

…………………………………………….

…………………………………………….

……………………………………………

**UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA**

Nathibitisha kuwa …………………………………………………………. (Jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa /kuandikishwa.

Baba yake (Jina kamili) ………………………………………………………………………… amezaliwa

katika mkoa wa ……………………………………………… Kata ya ……………………………………

Mama yake (Jina kamili) …………………………………………………………………………….

amezaliwa katika kata ya ………………………………. Tarafa ya ………………………………………

Wilaya ya …………………………………...………. hapa nchini.

NB: **Kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia hati hii kikamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa Mkuu wa Shule tarehe ya kuripoti shuleni.**

**.................**

**MKUU WA WILAYA**

**KIAMBATANISHO G.**

**FOMU YA KUMWANDIKISHA MWANAFUNZI SHULENI**

**(Jaza fomu hii kwa uangalifu)**

**1.** Jina kamili la mwanafunzi……..…………………………………………………………………
**2.** Tarehe ya kuzaliwa …………………………………Wilaya…………………………………….

**3.** Kabila ………………………. Uraia ……………………………………. Dini ………………...

**4.** Jina la mzazi…………………………………………………………………………………

Anuani ya mzazi ……………………………………………………………………………….

Kazi ya mzazi …………………………Simu Na 1……………………2……………………

---

(Sehemu hii ijazwe na wanafunzi ambao hawakai na wazazi wao)

**5.** (a) Jina la Mlezi ……………………………………………………………………………….

(b) Uhusiano kati ya mlezi na mwanafunzi ……………………………………………………

(c) Kazi ya mlezi ………………………………………………………. Simu Na……………
(d) Anuani ya mlezi

……………………………………………………………………………………

---

**6.** Shule atokayo mwanafunzi …………………………………………………………………
**7.** Wakati wa likizo mwanafunzi atakwenda wapi?

…………………………………………………...

**8.** Maelezo ya mwanafunzi

…………………………………………………………………………  ………………………………

……………………………………………………………………………………………….………

**9.** Ujuzi (Stadi) nyingine

……………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………

Saini ya mwanafunzi ………………………………………………… Tarehe ………………….

**KIAMBATANISHO H.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA JIJI MBEYA

*Baruazoteziandikwekwa*:

**Simu**:+25 250 3495

**MBEYA.**

*Email; **mbysecschool@yahoo.com***

Shule ya Sekondari Mbeya,
S. L. P. 372,

**Tarehe ……………….** Ref.

No. ………………

To Medical officer,

…………………………

## PART A

Mr./ Miss ………………………………………………………………………………………………

Please examine the above named student to his/ her physical and mental fitness for a full time student in this school. The examination should include the following categories:

1. Haemoglobin …………………………………………………………………………………
2. P. V. bleeding …………………………………………………………………………………
3. Sight: …………………………………………………………………………………………….
4. Blood pressure:

   ……………………………………………………………………………………...
5. Urine for sugar……………………………………………………………………..............
6. Stool for routine examination……………………………………………………………………….
7. Pregnancy test

   ………………………………………………………………………………………
8. Skin diseases …………………………………………………………………………….....
9. Leprosy ……………………………………………………………………………………….
10. Any deformity …………………………………………………………………………………
11. Epilepsy ……………………………………………………………………………………………..
12. Pulmonary tuberculosis ………………………………………………………………………
13. Neutosis ……………………………………………………………………………………….
14. Venerial diseases ………………………………………………………………………………
15. Other serious diseases ………………………………………………………………………

**PART B**

## MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a government medical officer)

1. I have examined the above named student and consider that he/ she is physically fit/ unfit and mentally fit/ unfit for a full time schooling.
2. Other comments: ………………………………………………………………………………
3. Date ………………..…Signature…………………………………………………………

   Station ………………………………………… Designation ………………………………

**Official stamp**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0768858548**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0755105938**
- **Mwandamizi Taaluma 054308684**
- **Mwandamizi Malezi 0763608875**